Msaidizi Ustawi wa Jamii Awamu ya Pili:

Stadi zinazotumika katika kuwasaidia watoto waishio katika mazingira hatarishi na familia zenye mahitaji maalum

Siku ya 1

Kushirikishana uzoefu

Usajili na jaribio la awali

Lengo la mafunzo

Kushirikishana uzoefu, kujenga na kuwezesha stadi zetu zinazohusiana na kutoa huduma kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi na familia.

Madhumuni

Ifikapo mwisho wa programu hii, washiriki wawe wameweza:

- Kuonyesha stadi zenye ubora zinazohusu utoaji huduma kwa watoto na familia, ulinzi wa watoto, kupunguza unyanyapaa, utetezi, na uwezeshwaji
- Kuelezea habari mpya kuhusu VVU/UKIMWI zinazohusu kufanya kazi na watoto na familia, sheria na sera
- Kushirikishana mafanikio na shauku zinazohusu kazi zao kama wasaidizi Ustawi wa Jamii na kupata mchango wa kina wa uzoefu wa kazi kutokana na utendaji wao
- Kupokea na kushirikishana habari kuhusu rasilimali zilizopo kwenye jamii na kitaifa ili kuwasaidia watoto na familia pamoja na kushughulikia mahitaji yatokanayo na VVU/UKIMWI

Shughuli za kukuwezesha kuwa msaidizi ustawi wa jamii

- Kupata mafunzo ya awali ya Usaidizi Ustawi wa Jamii: siku 9
- Kupata uzoefu kwa kufanya kazi chini ya usimamizi (miezi 6)
- Kupata mafunzo ya wasaidizi Ustawi wa Jamii awamu ya pili (Siku tano)
- Msaada wa ziada wa ufuatiliaji na menejimenti yenye ubora
- Kufikia mwisho wa mafunzo haya utakuwa umemaliza mafunzo ya wasaidizi Ustawi wa Jamii na utapata cheti cha kuhitimu mafunzo haya kama msaidizi Ustawi wa Jamii

Taswira ya Mafunzo

Siku ya Kwanza	Siku ya pili	Siku ya tatu	Siku ya nne	Siku ya tano	Siku ya sita
Kushirikishana uzoefu wetu	Taarifa mpya kuhusu VVU/UKIMWI	Kutathimini mahitaji maalumu ya mtoto na familia na uwezo wa familia kuhimili	Ulinzi wa watoto, unyanyasaji wa watoto na tathmini ya hatari	kuiwezesha wa jamii Kutunza kumbukumbu	Taarifa mpya kwa ajili ya msimamizi
Taarifa mpya za washiriki sKufanya kazi na serikali za mitaa na sheria ya mtoto ya 2009 Kushughulikia unyanyapaa na maswala ya jinsia	Kuvunja ukimya kuhusu VVU Watoto waishioathirika na VVU Kupunguza athari kwa watoto wakubwa	Kufanya kazi na familia kuwasaidia watoto Tathmini mpya Mahitaji maalumu Uwezo wa familia kuhimili	Ulinzi wa watoto, unyanyasaji wa watoto na tathmini ya hatari Sheria ya mtoto ya 2009	Kuiwezesha jamii Kutunza kumbukumbu za kazi ya tathmini zetu Utetezi wa haki za mtoto na ushirikishwaji wa mtoto Kufanya kazi na vikundi vya jamii	Mchakato wa kupanga mipango katika jamii Utetezi na uwezeshaji Uongozi kupata msaada kwa wasimamizi wa Ustawi Jamii

Utangulizi

- Kuwatambulisha Wawezeshaji
- Kuvunja Ukimya: Kutambulisha washiriki
  - Kujipanga katika vikundi vya watu wawili wawili. Kuzungumzia uzoefu wako kama Msaidizi wa Ustawi wa Jamii au Wasimamizi hadi sasa
    - Jina na mahali unakotoka?
    - Shughuli zipi unazozifanya kama msaidizi Ustawi wa Jamii au Msimamizi
    - Unatakiwa kufanya nini ili uweze kuboresha utoaji wa huduma?
  - Kila mmoja ajitambulishe kwa ufupi kwenye kikundi

Utunzaji wa Nyumba

- Kumchagua mwenyekiti, Katibu n.k
- Sheria za msingi

Kushirikishana uzoefu kutoka mafunzo yaliyopita

Mjigawe katika makundi manne . Mtumie bango kitita na kalamu ya wino mzito :

- Je nini kinatokea kwenye jamii yako kuhusu watoto waishio katika mazingira hatarishi?
- Je ni yapi majukumu ya wasaidizi Ustawi wa Jamii?
- Je ni mafanikio gani mliyoyapata mkiwa wasaidizi Ustawi wa Jamii?
- Je unaweza kufikiri mfano wowote wakati ambapo ulipata changamoto na ukahitaji msaada zaidi?
- Je unahitaji taarifa zipi za ziada au elimu?

Mrejesho

- ***Uwasilishaji wa kazi za vikundi juu ya:***
  - Majukumu ya msaidizi Ustawi wa Jamii
  - Mafanikio
  - Changamoto
  - Utakachohitaji siku zijazo

Mfumo wa uwasilishaji wa matukio

- Jina na umri wa mtoto
- Wanafamilia wengine
- Ni matatizo yapi yaliyotambuliwa**?**
- Tathmini ilifanyikaje? (Fomu za utambuzi,vitendea kazi vingine)
- Mpango wa utoaji huduma ulikuwaje?
- Matokeo yalikuwaje?
- Maswali yanayohitaji mjadala.

Kufanya kazi na serikali za mitaa

Kufanya kazi na serikali za mitaa

Je ni lipi jukumu la mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuwasaidia watoto waishio katika mazingira hatarishi na familia zao?

Kufanya kazi na serikali za mitaa

- Je muundo wa serikali ya kijiji hadi wilaya ukoje?
- Je wasaidizi Ustawi wa Jamii wana nafasi gani katika muundo?
- Je unawajibika kutoa taarifa kwa nani na wapi unakopata msaada?

Muundo wa Serikali za Mitaa na kazi zake- kufanya kazi na wasaidizi Ustawi wa Jamii

Bungua bongo

Mchoro unaoonyesha muundo wa SM



Je ni ipi nafasi ya wasaidizi Ustawi wa Jamii?

- ***Katika ngazi ya kijiji:***
  - Kufanya kazi na serikali ya kijiji kuwatambua watoto waishio katika mazingira hatarishi na miundo iliyopo inayofanya kazi na watoto waishio katika mazingira hatarishi kama vile kamati ya watoto waishio katika mazingira hatarishi (WWMH) na mashirika ya jamii
  - Kushirikisha taarifa na takwimu za watoto waishio katika mazingira hatarishi kwa uongozi wa serikali ya kijiji.
  - Tetea utoaji huduma kwa watoto wengi waishio katika mazingira hatarishi na familia zao
  - Shawishi na tetea maswala ya watoto waishio katika mazingira hatarishi ili yaingizwe kwenye mipango ya maendeleo ya kijiji.

Je ni ipi Nafasi ya wasaidizi Ustawi wa jamii? (inaendelea)

- ***Katika ngazi ya kijiji:***
  - shawishi na kutetea kushiriki katika kamati za maendeleo ya kijiji
  - Kushiriki katika mikutano ya hadhara ya kijiji. Mfano katika mchakato wa bajeti.Kutengeneza mtandao na watenda kazi wengine wanaofanya kazi na watoto waishio katika mazingira hatarishi kama ,waalimu, tabibu,viongozi wa dini, mashirika yasiyo ya serikali na mashirika ya jamii.

Nafasi ya wasimamizi wa wasaidizi Ustawi Jamii

- ***Katika ngazi ya Kata:***
  - Kuwatambulisha msaidizi Ustawi wa Jamii katika serikali zao za vijiji na kamati za maendeleo za kata
  - Kutoa taarifa za maswala na agenda za watoto waishio katika mazingira hatarishi katika kamati za maendeleo za kata
  - Kufanya ushawishi na utetezi wa agenda za watoto waishio katika mazingira hatarishi ili yawekwe katika mipango ya maendeleo ya kata
  - Kuwezesha mikutano ya utetezi kwa masuala ya watoto waishio katika mazingira hatarishi kwa msaidizi ustawi wa jamii na watu mashuhuri kwenye wadi. K.m. Diwani
  - Kufanya mikutano ya uhamasishaji kwa ajili ya viongozi wa kata na watu mashuhuri kama , viongozi wa dini na wastaafu.

Majukumu ya msimamizi wa wasaidizi Ustawi wa Jamii katika wilaya.

- Kutengeneza ripoti juu ya takwimu/ taarifa inayohusu WMH kutoka kwa wasimamizi wa wasidizi Ustawi wa Jamii na kuiwasilisha kwa kamati za menejimenti za wilaya.
- Shawishi na kutetea maswala ya watoto waishio katika mazingira hatarishi kwenye mipango ya maendeleo ya wilaya.
- Utafutaji wa rasilimali na uchangishaji wa fedha ili kutekeleza shughuli za watoto waishio katika mazingira hatarishi.

Kufanya kazi na serikali za mitaa

- ***Ni kwa jinsi gani serikali za mitaa zinafanya kazi na rasilimali zingine***
  - Watoa huduma za afya
  - Shule
  - Mashirika/asasi ya dini
  - Viongozi wa kisiasa
  - Polisi n.k.

Kufanya kazi na serikali za mitaa

- Kushirikishana mifano katika kundi kubwa jinsi wanavyofanya kazi na serikali za mitaa.

Je Serikali za Mitaa zina jukumu gani katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mtoto?

Leo tutaanza kujadili Swala hili mahsusi kuhusiana na jinsi tunavyofanya kazi na Serikali ya Mtaa
Katika siku ya 2 tutajadili Sheria na Ulinzi wa Mtoto kwa undani zaidi.

Je ni upi wajibu wa Serikali za Mitaa katika kusimamia Utekelezaji wa Sheria ya Mtoto?

- Wajibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuwalinda watoto na kuhamasisha upatanisho (Sehemu ya 94)
- Wajibu wa kuripoti ukiukwaji wa haki za mtoto (Sehemu ya 95)
- Uchunguzi unaofanywa na Idara (Sehemu ya 96)Amri ya Mahakama kuhusu matunzo kwa ajili ya kumnufaisha mtoto (Sehemu ya 18)
- Amri ya Mahakama kuhusu usimamizi (Sehemu ya 19)

Jukumu la kulinda na kuhamasisha ustawi wa Mtoto katika eneo lake

- Afisa Ustawi wa Jamii katika Serikali ya Mtaa ana wajibu wa kushughulikia ustawi wa watoto akisaidiwa na maafisa wengine wa Serikali za Mitaa.
  - Kutoa ushauri kwa wazazi wote, walezi, ndugu na watoto kwa kusudi la kuhamasisha kuwepo na upatanisho miongoni mwao.
- Kuwa na Daftari la Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi zaidi katika eneo husika na kuwapa misaada kila inapowezekana ili kuwawezesha watoto hao kukua kwa heshima miongoni mwa watoto wengine na kuendeleza uwezo walionao.

Jukumu la kulinda na kuhamasisha ustawi wa Mtoto (inaendelea)

- Kumsaidia mtoto yeyote anayehitaji msaada kutokana na kuwa amepotea, ametelekezwa au anatafuta hifadhi
- Kushirikiana na Polisi kuwatafuta wazazi, walezi au ndugu wa mtoto yeyote aliyepotea, au kutelekezwa na kumrejesha mtoto huyo mahali anapoishi na kupeleka suala hilo kwa Afisa Ustawi wa Jamii au kwa Afisa Maendeleo ya Jamii.
- Kumpa msaada mtoto yeyote aliyepotea au kutelekezwa au kutafuta hifadhi.

Jukumu la kuripoti ukiukwaji wa haki za mtoto

- Mwanajamii yeyote mwenye ushahidi au taarifa kuhusu ukiukwaji wa haki ya mtoto au kuwa mzazi, mlezi au ndugu mwenye jukumu la kumtunza mtoto ameacha kumpatia mtoto chakula, malazi, haki ya kucheza au mapumziko, mavazi, matibabu na elimu ni lazima atoe taarifa hiyo kwenye Serikali za Mtaa
- Afisa Ustawi wa Jamii anayepokea taarifa hiyo anaweza kumwita mtu anayetuhumiwa kulingana na taarifa iliyotolewa kwa ajili ya kujadili suala hilo na kufikia maamuzi muafaka kwa manufaa ya mtoto.

Jukumu la kuripoti ukiukwaji wa haki za mtoto

- Pale ambapo mtuhumiwa katika ripoti iliyotolewa anapokataa kukubaliana na uamuzi uliofikiwa, Afisa Usawi wa Jamii atawasilisha shauri hilo mahakamani. Mahakama inaweza kufanya yafuatayo:
  a. Kutoa ***unafuu*** wa namna yoyote au Amri kulingana na mahitaji ya mazingira yaliyopo
  b. Ikiwa mhusika ni mzazi, pamoja na **ahueni** au Amri iliyotolewa, ataamriwa kuweka dhamana kwa ajili ya kutoa matunzo na malezi muafaka kumpatia mtoto hitaji au mahitaji yake yote

Uchunguzi wa Idara

- Pale Afisa Ustawi wa Jamii anapokuwa na sababu za kutosha kuhisi kuwepo kwa unyanyasaji wa mtoto au hitaji la kutoa matunzo na ulinzi kwa mtoto, kwa kuambatana na Afisa wa Polisi anaweza kuingia na kufanya upekuzi wa makazi alipo mtoto ili kufanya uchunguzi
- Pale ambapo baada ya uchunguzi kufanyika imebainika kuwa mtoto amefanyiwa unyanyasaji au ana mahitaji matunzo ya dharura na ulinzi, Afisa Ustawi wa Jamii, akiandamana na Afisa wa Polisi atamchukua mtoto na kumpeleka mahali penye hifadhi salama kwa kipindi kisichozidi siku saba.

Uchunguzi wa Idara

- Pale mtoto anapokuwa amekosa makazi au ameondolewa kutoka makazi yake, Afisa Ustawi wa Jamii atapaswa kumleta mtoto mahakamani katika muda usiozidi siku kumi na nne ili Amri ya mahakama itolewe.
- Mahakama inaweza kuamua mtoto awekwe katika makazi maalum au chini ya uangalizi wa Afisa Ustawi wa Jamii au mtu mwingine yeyote mahakama itakavyoona inafaa mpaka pale shauri hilo litakapopatiwa ufumbuzi

Majukumu ya Afisa Ustawi wa Jamii

Sheria ya Uangalizi na Matunzo (Sehemu ya 20)

- Toa ushauri na unasihi kwa mtoto na familia yake;
- Kuwa na mapitio ya mara kwa mara na kupanga mipango ya baadaye ya mtoto kwa kushirikiana na mtoto mwenyewe, wazazi wake au mlezi;
- Kuiomba mahakama kutoa Amri au kuirekebisha amri hiyo iwapo italazimu na
- Kuchukua hatua muafaka kuhakikisha kuwa mtoto hapati madhara yoyote

Kuweka mkazo juu ya ulinzi wa watoto

- Afisa Ustawi wa Jamii ana jukumu la msingi kuleta maswala ya watoto wenye mahitaji ya ulinzi kwa kuijulisha mahakama

Kuweka mkazo juu ya ulinzi wa watoto

Mahakama inaweza kutumia aina mbili za amri kwa niaba ya mtoto mwenye mahitaji ya ulinzi :

- Amri ya matunzo au matunzo ya muda yaweza kumuondoa mtoto kutoka kwenye hali yeyote anayoteseka/ya mateso au yenye kuashiria mateso ya aina fulani na kuhamisha haki ya mzazi kwenda kwa afisa ustawi
- Amri ya usimamizi- -Usimamizi au amri ya muda ya usimamizi lazima ilenge kumuweka au kuzuia madhara ya aina yeyote yaliyosababishwa kwa mtoto ikiwa atabakia ndani ya familia anayoishi chini ya uangalizi wa mzazi, mlezi au ndugu.

Kushugulikia unyanyapaa ukiwa kama Msaidizi Ustawi wa Jamii

Rejea mada ya unyanyapaa kutoka katika mafunzo ya awali ya wasaidizi Ustawi wa Jamii

- Nini maana ya unyanyapaa ?

Maana ya unyanyapaa (rejea mafunzo ya awali kwa wasaidizi Ustawi Jamii)

- Unyanyapaa ni hali isiyokubalika kijamii kutokana na tabia za mtu, mazingira au imani iliyo kinyume na mila na desturi za jamii husika
- Ni chombo chenye nguvu cha kudhibiti jamii
- Hutumika kugandamiza, kubagua, kutumia nguvu dhidi ya watu waishio na tabia fulani
- Huwaathiri hasa watoto waishio katika mazingira hatarishi (“yatima”) na watu wanaoishi na VVU

Uzoefu wako ni upi kuhusu unyanyapaa ukiwa kama msaidizi Ustawi wa Jamii?

Mifano?

Hatua saba kwa ajili ya kupunguza unyanyapaa katika jamii kwa wasaidizi Ustawi wa Jamii

1. ***KUTAMBUA/KUBAINI:*** Hali yaunyanyapaa
2. ***KUJADILI:*** Madhara ya unyanyapaa kwa mtoto na familia.
3. ***KUPANGA:*** Tengeneza mpango kazi :
4. ***SAIDIA:***
   a) Jinsi ya kumsaidia mtoto na familia kukubali
   b) Utumiaji rasilimali
5. ***KUUKABILI:*** Kuukabili unyanyapaa
6. ***KUTOA TAARIFA:*** Tumia rasilimali za kisheria
7. ***HATUA:*** Tekeleza mpango

1. KUTAMBUA hali za unyanyapaa

1. Kuna mifano gani ya hali za unyanyapaa au ubaguzi
   Kwa vipi jambo hili linahusiana na VVU?

Mifano ya hali za unyanyapaa au ubaguzi unaohusiana na watoto waishio katika mazingira hatarishi na/au VVU?

- Kuwaita majina yasiyofaa
- Kukataa kumjumuisha mtoto pamoja na wengine kwenye kundi au shule
- Kupigana,vurugu
- Kulazimishwa kutoa taarifa
- Kukataa huduma
- Mengineyo??

Mifano ya hali za unyanyapaa au ubaguzi zinazohusiana na watoto waishio katika mazingira hatarishi na/au VVU?

- Tufanyeje (au wafanyeje) ili kuepuka unyanyapaa au kujilinda wenyewe pamoja na watoto wetu dhidi ya unyanyapaa?

Mifano ya hali za unyanyapaa au ubaguzi zinazohusiana na watoto waishio katika mazingira hatarishi na/au VVU?

- ***Sisi (au wengine) tufanye nini au tujilinde vipi pamoja na watoto wetu ili kujiepusha na unyanyapaa?***
  - Tusiongee kuhusu (VVU,hali ya uyatima,n.k.)
  - Kuuita kitu kingine
  - Kuikana hali
  - Kujiepushe na watu
  - Mengineyo ????

Mifano ya hali za unyanyapaa au ubaguzi unaohusiana na watoto waishio katika mazingira hatarishi na/au VVU?

- ***Sisi (au wengine) tunafanya nini au tunajilinda vipi pamoja na watoto wetu ili kujiepusha na unyanyapaa?(Inaendelea)***
  - Tafuta watu waadilifu wa kuzungumza nao
  - Pata taarifa zaidi
  - tujiepushe na hali za unyanyapaa
  - Tusiongee kuhusu (VVU, hali za uyatima,n.k.)
  - Kuuita kitu kingine
  - Ikatae hiyo hali
  - Jiepushe na watu
  - Mengineyo?????

2. KUJADILI athari za unyanyapaa kwa watoto na familia

- Ni kwa namna gani unyanyapaa unaweza kumuathiri mtoto?
- Kwa namna gani unyanyapaa unaweza kuiathiri familia au wale wanaomlea mtoto?

KUJADILI athari za unyanyapaa kwa watoto na familia

- Ni kwa namna gani unyanyapaa unaweza kumuathiri mtoto?
  - Huwa na sononi
  - Huwa mwenye Hasira
  - Hujitenga
  - Matatizo ya kitabia
- Kwa namna gani unyanyapaa unaweza kuiathiri familia au wale wanaomlea mtoto ?

  Kwa namna hiyohiyo

3. KUPANGA: Tengeneza mpango kazi

1. Tambua hatua maalumu za utekelezaji
2. Tambua NANI atafanya NINI na LINI
3. Ni asasi zipi za huduma zitahusishwa katika Swala la rufaa au ufuatiliaji?

4. Msaada: Jinsi ya kuwasaidia watoto na familia kuchukuliana na hali iliyopo

Ni kwa njia gani nyingine tunaweza kumsaidia mtoto kuchukuliana na hali iliyopo?

Msaada : Jinsi ya kumsaidia mtoto na familia kukabiliana na hali

Ni kwa njia zipi zingine tunaweza kumsaidia mtoto kuweza/kukabiliana na hali?

- Kumsikiliza mtoto maswala aliyo nayo
- Kuwauliza wanaendeleaje
- Wape taarifa
- “Kuifanya hali iwe ya kawaida ”– jinsi inavyoweza kutokea hata kwa wengine pia.
- Kuwasaidia kutengeneza mpango wa utakaowasaidia
- Mengineyo?

Jinsi ya kuwasaidia watoto na familia kukabiliana na hali

Misaada gani mingine inayoweza kutolewa?

- Kuwaomba wanafamilia kusaidia? Kwa njia gani? Kuwatambua watu wengine wanaoweza kusaidia zaidi.
- Kusaidia kupanga kwa ajili ya maisha ya “kawaida” ya baadaye – elimu, mafunzo ya kazi, n.k.
- Mengineyo?

5. KUPAMBANA: kupambana na unyanyapaa

Tutamsaidiaje mtoto na familia kukabiliana na unyanyapaa?

- Kuielimisha jamii
- Kuzungumza na mtu anayesababisha unyanyapaa
- Kupeleka malalamiko
- Mengineyo?

KUPAMBANA: kupambana na unyanyapaa

- msaidizi ustawi wa jamii husaidia kutambua ni nani wa kukabiliana naye
- Kuchagua namna ya kupeleka malalamiko au kumwomba mhusika aache tabia ya kunyanyapaa
- Kumuandaa mtoto au wanafamila kuchukua hatua
- Kuwasaidia kueleza jinsi ambavyo unyanyapaa unawaathiri(tumia kauli”mimi”)
- Kusaidia ufuatiliaji

6. KUTOA TAARIFA: Tumia rasilimali za kisheria

- Hali zipi za unyanyapaa ziko kinyume na sheria?
  - Vurugu
  - Kukataa kazi au huduma
  - Kubaguliwa kunakohusishwa na VVU?
  - Mengineyo??
- Tunapataje msaada wa kisheria?

7. KUCHUKUA HATUA: Utekelezaji wa mpango

Je nini kimetokea? Kupitia Upya Mpango

(Kuutathmini mpango)

Mazoezi ya Kikundi kwa kutumia hatua 7

Mazoezi ya Vikundi kupunguza Unyanyapaa kwa kutumia matukio katika uzoefu wako

- Mjigawe katika makundi manne
- Chagueni tukio mlilolifanyia kazi na kwa kuanzia onyesheni ushahidi wa unyanyapaa na chanzo chake
- Fanyeni majadiliano ya athari zake kwa mtoto na familia
- Igizeni namna familia inavyoweza kusaidia /au kuchukuliana na hali hiyo
- Igizeni namna wanavyoweza kukabiliana na chanzo cha unyanyapaa na athari zake
- Igizeni namna vyanzo halali/vinavyokubalika vinavyoweza kupatikana
- Kutokana na kujifunza hatua za kuchukuliana, kukabiliania na kutoa taarifa andaeni Mpango kazi
- Fanyeni majadiliano kuhusu mliyojifunza kutokana na matumizi ya stadi na hatua za modeli ya kupunguza unyanyapaa

Jinsia na Huduma za msaidizi Ustawi wa Jamii

Mawazo yetu kuhusu Jinsia yanawezaje kuathiri misaada kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi na familia zao?

Bungua bongo

Wanawake na Wanaume na msaidizi Ustawi wa Jamii

- Wanawake wengi hawashiriki sawia au kikamilifu katika maamuzi ya kifamilia
- Wanawake wengi hawana fursa sawa ya kupata raslimali za familia, zikiwemo fedha, ardhi na raslimali nyingine kama vile chakula wakiwa kama wake au wajane
- Wanawake wengi hawana hadhi sawa na waume zao katika maisha yao ya unyumba au hata katika afya ya uzazi
- Wanawake wengi hutanguliza mahitaji ya watoto wao kabla ya mahitaji yao binafsi
- Wanawake wengi huangukia katika kunyanyaswa, kudharauliwa, magonjwa na hawana nafasi sawa ya kupata elimu au fursa nyingine za kiuchumi

Nini maana ya kutokuwa uwiano wa kijinsia na ni kwa namna gani unatuathiri sis na kazi zetu?

Jadili

Mjadala kuhusu kutokuwepo kwa Usawa wa Kijinsia

Ukosefu wa usawa wa kijinsia unaathirije afya ya jamii kwa ujumla na hali ya uchumi wa familia?

- Je kuna usawa wa jinsia katika familia?I
- Kutokuwepo kwa Usawa wa kijinsia kunaathirije mawasiliano ya familia na mazungumzo ya unyumba?
- Ukosefu wa usawa wa kijinsia unaathirije hatari ya maambukizo ya VVU katika familia?
- Ukosefu wa usawa wa kijinsia unaathirije maendeleo ya wasichana tangu utoto hadi utu uzima?
- Ukosefu wa usawa wa kijinsia unaathirije maendeleo ya wavulana tangu utoto had utu uzima?

Je msaidizi Ustawi wa Jamii anaweza kufanya nini kushughulikia maswala ya kijinsia?

- Kusikiliza kwa makini: Kujaribu kuelewa jukumu la wanafamilia mbalimbali kuhusu Swala la jinsia
- Kuuliza maswali kutambua kama wanawake na watoto wanaridhishwa na majukumu yao na shughuli zao katika familia na jamii na inakuwaje kuhusu wanaume.
- Kutoa taarifa na elimu kuhusu baadhi ya mibadala ya majukumu, shughuli na taratibu za kimila.
- Kuweka viunganishi kwa raslimali na shughuli zilizopo zinazoweza kutumiwa na familia kuleta mgawanyo mzuri zaidi wa majukumu na njia mbalimbali za matunzo na misaada.
- Tumia kielelezo cha hatua saba za unyanyapaa kushughulikia unyanyapaa na ubaguzi unaohusiana na jinsia.

Muhtasari na Mrejesho wa Siku

Majumuisho ya Kuhitimisha na Kupongezana